## Kichwa cha mafundisho : **NITALIJENGA KANISA LANGU.** (Mat. 16:18)

**Kwa kuwa mtu anapookoka hawekwi na kuishi mahali pengine isipokuwa katika Kanisa la Kristo, somo hili litatusaidiya kutafakari kuhusu lile Kanisa Kristo alisema atajenga na kujiswali kuhusu lile unamoshiriki na kuhudumu ili ufanye uamzi ulio bora.**

Mafundisho haya yametolewa na Kanisa la Kristo pa Bukavu
76, Av. Industrielle, Bukavu – DRC.

## I. MPANGO WA KRISTO

***18*** *''Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, hata malango ya kuzimu hayataweza kulishinda.* (Mat. 16:18)

Aliyesema haya ni Yesu Kristo. Katika hili andiko, mitume walitakiwa kutowa ripoti ya mahali popote ambapo Yesu alipita akifundisha na kufanya miujiza. Lengo moja kati ya zingine ni kuhakikisha kwamba kati yao wote, kuna wale wanaomjuwa.

Basi swali lilitumwa kwa nani ? Ni kwa wale wa nje na mitume pia.
Nyuma ya kusikia majibu ya wale wa nje ("*Baadhi ya watu husema ni Yohana Mbatizaji, wengine husema ni Eliya na bado wengine husema, ni Yeremia au mmojawapo wa manabii.*''), Yesu anataka kuhakikisha kwamba mitume wake wanamjua wala nao watamfananisha. Ndipo mmoja wao, yaani Petro, akasema : "*wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai*". Yesu akahakikisha haya kwa kuongeza : "***17****...Heri wewe, Simoni mwana wa Yona, kwa maana hili halikufunuliwa kwako na mwanadamu, bali na Baba yangu aliye mbinguni.* ***18***
*'Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, hata malango ya kuzimu hayataweza kulishinda."* Aaaamen!!!!
Tunasimamiya kwa hayo, zaidi kulingana na lengo la somo hili.

Lazima nasi tumjuwe vizuri Kristo bila kumfananisha, pia tulijuwe kanisa lake (ambao ni mwili wake) bila kulifananisha. Katika somo hili, tunakwenda kuligundua kanisa la Kristo bila kulifananisha. Endapo msomaji atalitambua vizuri, atapata kufikiri maradufu kuhusu lile anamo shiriki, huku akijiuliza : Je, hii ndiyo picha ya Kanisa la Kristo kama vile alivyolipangilia ? Je, amesema kwa uwingi wala kwa umoja ? Sasa, kupitiya maneno yake, tumeona ya kwamba ni kwa umoja (maana ya universal) ndipo amesema. Lazima viungo vyake (kanisa za mahali) vifanane kabisa.
Yesu alipokuwa bado hai, alisema atalijenga kanisa lake kwa muda utakaokuja. Kwa hiyo ahadi, Yesu akahakikisha lengo lake halisi : kulijenga kanisa lake yaani kundi la watu watakaokuwa na mhuri wake pia watakaoitwa kwa jina lake. Hapa ni wazi kuwa kanisa la Kristo silo jengo watu wanalojijengeya ila ni watu walio milki (mali halisi) yake.
Katika Biblia, haiwezekani kutenganisha kazi ya Kristo na ya Kanisa lake, kama vile ni vigumu kutenganisha mwili mzima na kichwa. Kama hili lingetendeka, mutu kama huyu angekuwa amekufa. Kwa hiyo, Paulo analiita « **mwili wa Kristo** » ili kuunganisha mtu na kazi yake: Efe.1 :22-23. Katika mpangilio wa Kristo, kulipashwa kuwa Kanisa moja tu. Biblia inasema katika Waefeso 4 :4-6


**Anuani za sasa**
N°76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
**BP** : 452, Cyangugu – Rwanda
**Email** : egliseduchristrdcbkv@yahoo.fr (français), klk.bukavu@yahoo.fr (swahili) et bkvdrcchurchofchrist@yahoo.fr (anglais).

« *4Kuna mwili mmoja na Roho mmoja, kama vile mlivyoitwa katika tumaini moja. 5Tena kuna Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja, 6Mungu mmoja ambaye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote, katika yote na ndani ya yote.* »
Sasa, alipofikiriya mwili mmoja (na wengi wanahakikisha hili), basi viungo visivyo fanana vimetoka wapi ? Ni mpango wa Mungu ao wa watu ? Ni wazi kuwa si mpango wa Kristo.

***Mfano*** : fikiriya kwanza mwanadamu ambaye unamkuta akiwa na :

- kichwa cha mtu,
- mikono ya kima,
- kiwiliwili cha samaki,
- miguu ni ya ndege.

Nafikiri, hutadanganyika kumwita « monstre » maana yake kiumbe fulani kisichowahi kuonekana katika dunia hii bali hataitwa mtu. Vivyo hivyo, kanisa la Kristo lilipashwa kuwa na viungo vinavyofanana, ila tunakuta:

## II. MAMIA NA MAELFU YA « MAKANISA » MBALIMBALI

Leo katika kila kona (pembe) ya dunia, tunakuta mamia na maelfu ya makanisa na wengi woa wanajidai « makanisa za Kristo ». Si vibaya kabisa ikiwa wote wangefanana na lile kanisa la Kristo lililoanza katika Agano jipya. Kristo aliomba sana ili "*wote wawe umoja*", hata lengo la Mungu ni « watu wote waufikiye wokovu » huu mkubwa kwa njiya ya Yesu Kristo peke yake wakiwekwa katika kanisa lake. Wanapouzarau, watapataje kupona ?
Ni nini imetukia ? Kristo ameshindwa kuufikiya ukomo wake ? Je, Kristo ametoa mpango na matumizi tofauti kiasi kusema kila mumoja ajenge kanisa la kwake, huduma (ministries, ministère) ya kwake, bora tu watu wafurahi na waje wengi? Katika shabaha ya kuleta majibu kwa haya maswali, tutachunguza Kanisa kama vile tunalikuta katika Agano Jipya, yaani katika Neno la Mungu.

***Mfano***: katika maisha, kunakuwa na wakati ambapo mtu anapoteza rafiki ao ndugu (siyo kupoteza kwa kufa ila katika mazingira, ikijulikana ya kwamba yeye bado hai). Ili uhakikishe ya kwamba ni yeye amepatikana huku wala kule, ama tena kwa shabaha ya kusaidiwa katika utafiti, kuna alama fulani ambazo zitakuwa kama kitambulisho cha mtu yule. Hata mwingine mtu akitambua zile alama, atahakikisha ya kwamba ndio ule mtu anayetafutwa. Atamleta na kumkabidhi kwa mhusika (rafiki wala ndugu). Vivyo hivyo, tukiwa na alama za kulitambua kanisa halali la Kristo, itakuwa ni rahisi kuchhagua la kweli na kuachana na la uongo (bandia).

## III. *Yaliyo ya kweli:* KANISA LA KRISTO KATIKA AGANO JIPYA NA ALAMA ZA KULITAMBUA.

Tumesema hapo mbele ya kwamba, leo kuna "makanisa" mengi katika ulimwengu huu. Je, miongoni mwao, ni rahisi kulitambua lile la kweli na lile bandia (lisilo la kweli)? Je, ni wale wasomi tu ndio wanaweza kuligundua, huku wengine wote wakifuata kama kondoo apalekwao machinjoni, wakisema eti hakuna mahali


**Anuani za sasa**
N°76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
**BP** : 452, Cyangugu – Rwanda
**Email** : egliseduchristrdcbkv@yahoo.fr (français), klk.bukavu@yahoo.fr (swahili) et bkvdrcchurchofchrist@yahoo.fr (anglais).

ambapo Mungu hayupo? (wakimaanisha wanaweza hudumu mahali popopte pale ambapo panatajwa Jina la Kristo). Je, ni lazima niwe (uwe) na kipawa special kwa kulitambua?

*Jibu ni moja*: tunapochukua zile alama za Kanisa la Kristo katika Agano jipya, yeyote atakuwa na uwezo wa kuligundua kirahisi mahali popote pale ambapo linapatikana.

Halitegemeyi uraiya, rangi, kabila, ukoo, elimu za dunia, ... ila linategemea Agano jipya ambamo limetajwa mara ya kwanza na Kristo na pia humo ndimo limeonekana waziwazi.

- (Mt. 16:18): Nitajenga *Kanisa* langu.
- (Mdo. 2:42): Bwana aliongezea *Kanisa* wale waliokuwa wakiamini.
- (Mdo. 15:41): Paulo alihimiza *Kanisa*.
- (Mdo: 20:28): Maaskofu wakilisha *Kanisa* la Bwana.
- (Rom. 20:28): Salimuni *Kanisa* lililoko nyumbani kwao.
- (2Kor. 11:28): Huzuni ninayokuwa nayo kwa ajili ya *Kanisa*.
- (Efe. 1:22): Kristo Bwana wa *Kanisa* ambaye ni mwili wake.
- (Efe. 5:24): *Kanisa* linamtii Kristo.
- (1Tit. 3:15): *Kanisa* la Mungu aliye hai.
- (Ufun. 1:4): Kwa *maKanisa* saba za Azia.
- Na kadhalika.

Kwa hiyo, vitambulisho halisi vya Kanisa la Kristo vipo katika Agano jipya, navyo ni vifuatavyo:

1. **Kanisa liliahidiwa** kujengwa na Kristo (Mt. 16:18) "***18*** *'Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, hata malango ya kuzimu hayataweza kulishinda.*" Hapa tunaona ya kwamba Kanisa ni mali ya Kristo tena ni mwili wake ambao hatuwezi fananisha na mwili mwingine wowote. Kama vile kila mtu ana mwili wake wa kipekee ambao Mungu amemupa, pia Kanisa la Kristo lina hali yake ya kipekee, tukichunguza mandiko wala si akili zetu ao tena hali ya kisasa.
2. Kanisa la Kristo **lilianza onekana** hapo Yerusalem siku ya Pentekoste. Luka 24: 45-49 na Mdo. 2:5. Hii haimaanishi kwamba liitwe "kanisa la kipentekoste" bali tu "kanisa la Kristo". Yaani, lilianziya kazi Yerusalem.
3. Kanisa la Kristo **lilianza kazi** yake munamo mwaka wa 33 kisha kuzaliwa kwa Yesu Kriso. Hii inatokana kwamba Kristo alianza huduma hadharani akiwa na miaka yapata 30 (Lk. 3: 23) na huduma yake ilidumu miaka tatu. Siku 50 tuu kisha Yeye kufufuka, mitume walipata nguvu mpya siku ya Pentekoste na hapo wakaanza tangaza Habari njema ya Yesu Kristo wakisema lazima watu watubu na kubatizwa ili wapate ondoleo la dhambi zao (Mdo. 2:38).
4. Kanisa liliitwa kwa **jina** la Kristo wala si kwa jina jingine, yaani **Kanisa la Kristo** ama tena **Kanisa la Bwana**, **Kanisa la Mungu**. Kanisa kama vile mwili wa Kristo, ni moja. Ila, lina vikundi vya mahali ambavyo vitaitwa kwa lile lile jina moja. Paulo aliposema "*makanisa yote ya Kristo yanawasalimu ninyi*", hamaanishi "makanisa" kwa majina tofauti kama ilivyo leo. Ndipo katika


**Anuani za sasa**
N°76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
**BP** : 452, Cyangugu – Rwanda
**Email** : egliseduchristrdcbkv@yahoo.fr (français), klk.bukavu@yahoo.fr (swahili) et bkvdrcchurchofchrist@yahoo.fr (anglais).

1Kor. 12:27 anasema: "*Basi ninyi ni mwili wa Kristo, na viungo vya mvili huu, mumoja mumoja*". Basi, mwili anaomaanisha ni nini? Ni Kanisa la Kristo kwa ujumla (Efe. 1:22-23).

5. Waliowekwa ndani ya Kanisa na Bwana, waliitwa kwa jina **wakristo**. "*... na ilikuwa kwa muda wa mwaka mzima wakakutanika pamoja na Kanisa, na kufundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa <u>wakristo</u> kwanza katika Antiokia*". Mdo. 11:26. "*Na Agrippa alimwambiya Paulo: kwa maneno machache unazani kunishawishi kuwa <u>mkristo</u>?*" Mdo. 26:28. "*Lakini mtu akiteswa kwa sababu yeye ni <u>mkristo</u>, asione haya; lakini atukuze Mungu katika jina hili*". 1Petr. 4:16. Jina hili halina lazma ya kingine kielelezo ili kujitambulisha zaidi. Linatosha na linamupa Kristo utukufu.

6. Kanisa la Kristo lina **kichwa kimoja** yaani Kristo mwenyewe. "*Naye ni Kichwa cha mwili ulio Kanisa; aliye mwanzo, muzaliwa wa kwanza kutoka katika wafu; ili apate kuwa wa kwanza katika yote*". Kol. 1:18. Hakuna vichwa viwili juu ya mwili mmoja, wala hakuna kichwa cha kutengenezwa na mwanadamu kinachostahili juu ya Mwili huu wa kipekee wa Kristo. Ni mshangao tunapowasikia wengine huhakikisha eti Kristo alisema atajenga kanisa lake juu ya Petro na hao wanajiwekeya mababa zao wenyewe. Kwa nini Kanisa la Kristo litegemeye mwanadamu japo Biblia yenyewe inasema "*alaaniwe amtegemeyaye mwanadamu*"? Hii haiwezekani hata kidogo.

7. Mwili wa Kristo (**Kanisa**) **ni mmoja tu**. "*Mwili ni mumoja, na Roho moja, kama vile mulivyoitwa katika tumaini moja la mwito wenu*". Efe. 4:4. Basi, ikiwa mwili ni mumoja, ni wazi kuwa Kanisa la Kristo ni moja tu nalo ni KANISA LA KRISTO. Kuna madhehebu yanayokiri "kanisa moja takatifu" huku wakimaanisha dhehebu lao. Kanisa la Kristo si dhehebu wala mgawanyiko wowote.

8. **Kukubaliwa** na Bwana katika kanisa lake si kama vile kuvuta rafiki na ndugu nyumbani mwa mtu. Hatua ambazo zinahitajika kupitiya ni wazi katika Agano jipya kwa kuwa wengine walizipitiya.

   Hatua ao tena shurti hizo ni zifuatazo:

   a. Kusikia Neno la Mungu yaani Habari njema na liguse moyo: Rum. 10:17; Mdo. 2:37.
   b. Kuamini Neno hilo ambalo linatuita kwenye wokovu: Mdo. 4:4; . 11:6; Heb. 10:14
   c. Kuamua kubadili maisha (mafikiri na nia ao kuacha njia mbaya) maana yake roho huzaliwa upya, kutubu na kuacha matendo ya zamani yasiyopendeza Mungu. Mdo. 2:38; Mdo. 17:3.
   d. Kukiri Kristo kama Mwana wa Mungu aokowaye peke yake. (Mdo. 9: 37; Rum. 10: 9-10).
   e. Kubatizwa kwa ubatizo wa kibiblia. Mko. 16-16; Mdo. 8:38.

Mtu anapopitiya hizo hatua, huongezwa na Bwana (Mdo. 2:42) wala si kujiingiza (kujipenyeza) ao tena kuingizwa na watu (wazazi, ndugu, mshirika, ..).


**Anuani za sasa**
N°76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
**BP** : 452, Cyangugu – Rwanda
**Email** : egliseduchristrdcbkv@yahoo.fr (français), klk.bukavu@yahoo.fr (swahili) et bkvdrcchurchofchrist@yahoo.fr (anglais).

9. **Ibada** ya Kanisa la Kristo ipo wazi katika Agano jipya. Wakristo walikusanyika kwa ibada **siku ya kwanza ya juma** (2Kor. 16:2). Wanaweza wakachukuwe zingine siku katika juma kw akujifunza Neno la Mungu ao mpango mwingine kwa mafundisho (Mdo. 19:9). Yale waliyoifanya wakati wakikusanyika ni:
   - **Kuimba** (Efe. 5:19; Kol. 3:16; Heb. 2:12; Heb. 13:15). Hii kuimba haikumaanisha kutumia vyombo vya muziki kwa kuwa ni kuenda kinyume na hiyo ibada ya Kanisa la Kristo katika Agano Jipya. Popote ambapo kuimba kunatajwa katika sehemu hii ya Biblia, vyombo vya muziki havitajwi kabisa. Ndipo wengi leo, kwa kutafuta kuviteteya eti ni halali katika ibada, wanarudi katika Agano la kale wakitaja Zaburi za Daudi. Basi, ikiwa tutasema ya kwamba yote yaliyo katika Agano la Kale tunaweza kuyafanya katika ibada ya leo, imetupasa tena kuunguza uvumba (encens), imetupasa kuteketeza wanyama kama sadaka, nakadhalika. Wengine husema eti kutakuwa na nyimbo na vigelegele mbiguni. Ni kweli, ila tujiulize, tunaweza tukafanye yote yatakayokuwa mbinguni hapa duniani? Kwa nini wachague tu vyombo vya muziki na kuacha mengine? Isitoshe, wengine husema eti hakuna ubaya kabisa kuvitumiya ao tena inapendeza na kuburudisha. Kwa hawa tujiulize kama cochote kinachopendeza machoni pa watu (yaani si kibaya kabisa ao kinaburudisha) tukilete katika ibada ya Kanisa la Kristo? Mbone itafananishwa na sadaka ya sauli? (1Sam. 15:22-23). Inabidi tufuate kwa uaminifu Agano Jipya ambamo Kanisa la Kristo lilianziya na ndimo lipo leo ili tujuwe yale yanayomupendeza Kristo wala si wanadamu. Mtu mumoja aliwahi sema: "ikiwa mtu atakuwa na vyombo vya muziki nyumbani kwake kwa sherehe fulani wala kujiburudisha, haimaanishi kuvikubali na kuvitumia katika ibada ya kanisa la Kristo".
   - **Kuomba** (Mdo. 2:42; Efe. 6: 18-19) kwa jina la Yesu Kristo.
   - **Kusoma na kujifunza Neno la Mungu** kwa shabaha ya kulitii (2Tim. 2:15; Mdo. 11:26; Mdo. 17:11; 1Thes. 5:21).
   - **Kuvunja mkate** wala kuyakaribiya meza ya Bwana kwa nia ya kutangaza kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo. (1Kor. 11: 23-32; Mdo. 2:46; Mdo. 20:7). Kwa kipindi hiki, wengi husema eti hapohapo mkate unageuka mwili wa Yesu Kristo na kikombe hugeuka damu ya Yesu Kristo; ijapokuwa ni kumbukumbu ya mwili na damu ya Yesu Kristo vilivyotolewa msalabani kwa ondoleo la zambi zetu.
   - **Kutoa sehemu ya mali zetu** kama changizo kwa mahitaji ya Kanisa la Kristo kwa ujumla na kwa kusaidiya wasiojiweza (ndani na hata nje ya kanisa). 1Kor. 16: 1-2; 2Kor. 8:1-4; Mdo. 11: 29-30; Heb. 13:16; Rum. 12:8; 2Kor. 9:5.

Tambua ya kwamba hakuna mahali mitume walilipisha au kulazimisha watu watowe kama vile tishiyo fulani. Pia, hizo sadaka nyingi za Agano la kale hazitajwi, mfano: moja ya kumi, malimbuko, sadaka ya shukrani, sadaka ya ukingo, nk. Wanaofundisha wakristo kutoa hizi zote, wanasahau kama utendaji wetu katika Kanisa la Kristo unategemea Agano jipya bila kusahau Agano la kale ambamo muna mifano ya kutuhimiza bali siyo kutenda kamili yale walitenda. Kama sivyo,


**Anuani za sasa**
N°76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
**BP** : 452, Cyangugu – Rwanda
**Email** : egliseduchristrdcbkv@yahoo.fr (français), klk.bukavu@yahoo.fr (swahili) et bkvdrcchurchofchrist@yahoo.fr (anglais).

tungekubali hata mkristo kuwa na wake wengi (zaidi ya mmoja) sawa na mifano mingi katika Agano la kale.

10. **Mafundisho muhimu** ya Kanisa la Kristo yanatoka katika **Neno la Mungu**. Vitabu hivi vina sehemu mbili: Agano la kale (Torati na manabii ambavyo Kristo alikuja kutimiza na kukamilisha) na Agano jipya (ndilo tumepewa kupitiya kifo cha Yesu Kristo msalabani kwa ajili ya dhambi zetu hapo alipomwanga damu yake. Hili ndilo Agano Mungu alifanya na wakristo, ndio maana tunahitajika kulishika kwa utendaji wa imani yetu tukiongozwa na Roho Mtakatifu). Hakuna mtu yeyote, hata malaika anao ruhusa ya kuongeza wala kupunguza kwa Neno la Mungu ambalo limekwisha andikwa na kukubaliwa mara moja.(Ufun. 22: 18-19; Gal. 1: 6-11) Kredo ao mielekeo za imani za zaidi zote za kutoka kwa wanadamu ni za kupigwa marufuko kwa kuwa ni kinyume na mapenzi ya Mungu na yale mitume waliishi katika Agano Jipya.

11. **Maongozi ya Kanisa la Kristo** ni wazi sana, tukifuata Agano jipya.
    - Kristo ndiye Kichwa cha mwili mzima (Efe. 5:23).

      Huu mwili una viungo (ambavyo ni makanisa za mahali zinazokusanyika zaidi manyumbani mwa wakristo), na viungo hivyo vinaongozwa na:
    - Baraza la wazee: Mdo. 14:23, Tit. 1:5. Wanaitwa pia maaskofu (Mdo. 20:28) ao tena wachungaji (1Petr. 5:3-4). Kazi zao ni: Kukesha juu ya Kundi la Bwana (Mdo. 20, 28-31; Heb. 13:17); kukamilisha watakatifu (Efe. 4:12); kuonya wakristo (1Tes. 5:12-15); kuwatunza kondoo wa Bwana (Mdo. 28:28; 1Petr. 5:1-3); na kuombeya wagonjwa (Yak. 5:13-18); Katika Kanisa la Agano jipya, hakuna mwanamke tumewahi kusikiya akifanya kazi kama mzee, askofu na mchungaji. Yanayotendeka leo imetokeya wapi, ao wameyasikiya mandiko vibaya (inayosema: *28Wala hakuna tena Myahudi au Myunani, mtumwa au mtu huru, mwanaume wala mwanamke, maana nyote mmekuwa wamoja ndani ya Kristo Yesu.* Gal. 3:28).
    - Washemasi: Mdo. 6:1-6; 1Tim. 3: 8-13.

    Katika kutangaza Neno la Mungu na kulifundisha, kunakuwa na Wainjilisti na Walimu. Katika Kanisa la Agano jipya.

    Ni vema tujuwe ya kwamba kanisa la Kristo halina:
    - mkurugenzi yeyote “mheshimiwa, wa kuabudiwa” wa hapa chini duniani,
    - makao rasmi,
    - wingi wa vyeo kama makundi mengi ya kisasa (ajabu kusikiya hata “archbishop” yaani mkubwa kuliko wachungaji wengine wote, na vinginevyo visivyokuwa katika Agano jipya).

12. **Kazi** ao **huduma ya kanisa la Kristo** ni ya aina tatu:

a. kuihubiri injili (Mk. 16: 15-16)

b. kuhimiza wakristo (Heb. 3: 12-14).

c. Kusaidiya wasiojiweza, wenye mahitaji (Mdo. 11: 29-30; Gal. 6: 1-10; Yak. 2: 14-22).


**Anuani za sasa**
N°76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
**BP** : 452, Cyangugu – Rwanda
**Email** : egliseduchristrdcbkv@yahoo.fr (français), klk.bukavu@yahoo.fr (swahili) et bkvdrcchurchofchrist@yahoo.fr (anglais).

Mtego ambao umeingiya na umewanasa wengi, ni hapo kanisa linapojishughulisha na miradi ya maendeleo kana kwamba ni moja ya kazi zake. Hii miradi inawavuta “wakristo bandia” (wasio wa kweli) ambao ni chanzo cha mchanganyiko katika kanisa la Kristo. Kwa ajili ya miradi hiyo, wengine huwekeyana chuki na fitina kiasi hata kuangamizana kufuatana na matumizi ya hiki na kile (pesa, gari, vyombo, mipango, watu, ofisi, nk.)
Ikiwa mradi wa maendeleo utamilikiwa na watu ambao wamejaa Roho Mtakatifu na Neno la Mungu, si vibaya. (hapa tunatowa maoni kama wanadamu) Ila tena, ni vizuri mambo yote yajadiliwe nje ya Kanisa la Kristo ambalo lina mpango na kazi zake za kipekee.

13. Yeyote ambaye ni **mkristo anashurtishwa kuishi maisha ya uaminifu na Kristo** (yaani mafundisho yake pamoja na ya mitume wake, pia yote ambayo yamekubaliwa na kuwekwa katika Biblia halali). Mkristo ni vema kupenda dunia na mambo yaliyomo kusiwe ndani mwake. Hapo upendo wa Mungu utatoweka ndani mwake. 1Yoh. 2:15; Yak. 4:4.

Mkristo aliyeongoka (aliyaokolewa), ni sherti:

- Atowe matunda ya roho (Gal. 5: 22-23).
- Asome Neno la Mungu kila siku na kulitafakari kwa shabaha ya kuliishi,
- Awe mwaminifu kwa Kristo (Mdo. 11:23) hadi mwisho ili atarajiye kuipokea taji ya uzima (Ufun. 2:10)
- Awe na mwenendo unaoshuhudiya kama yeye ni mfuasi wa Kristo (Flp. 1:27): katika mazingira anamoishi, katika ndoa yake, nyumbani anamoishi, mahali anaposhughulika na kazi za mikono, katika masemi yake, …
- Awe na maisha iliyo hai (kama jiwe hai) katika Kanisa la Kristo,
- Awe mwenyi kupenda mashauri mema na kuyatafuta kwa watumishi wanaojaa Neno na Roho Mtakatifu,
- Awe mwenyi kuchukiya na kujitenga na mashauri ya wasiomcha Mungu pamoja na faida zisizodumu na za ubatili,
- Awe mwenye kuuweza na kuutiisha mwili wake pamoja na nia chini ya Neno la Mungu ili asipelekwe na mambo ipendezayo walimwengu,
- Awe mwenye kujitayarisha kila siku kwa kuwa hakuna ajuwaye siku ya kurudi kwa Bwana ili kuchukuwa walio wake,

Kwa kweli, mashauri ya kutolea ni mengi ila haya machache yakishikwa, mtu wa Mungu atasimama imara katika imani safi.

## IV. HITIMISHO NA MASHAURI MEMA KWA MSOMAJI

Ni alama kumi na tatu ndizo zimetajwa ili kukusaidiya, ndugu mpenda, kulitambua kanisa la Kristo la Agano Jipya. Basi, endapo utakuwa umezigunduwa na kuzihakikisha, ni wajibu wako kujuwa ya kwamba ni ujinga wako kuligan’ganiya kanisa ambalo halifanani na lile la Kristo. Ikiwa lile unamoshiriki halionyeshi alama hizi zote, utajaza mwenyewe ni la nani. Labda ni la watu wamejitungiya kwa lengo la kupata kazi, pesa, sifa, waumini, wasiwe wenyewe ndio wataangamia, … wakitumikisha watu kama watumwa, japohiyo Yesu


**Anuani za sasa**
N°76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
**BP :** 452, Cyangugu – Rwanda
**Email :** egliseduchristrdcbkv@yahoo.fr (français), klk.bukavu@yahoo.fr (swahili) et bkvdrcchurchofchrist@yahoo.fr (anglais).

anapenda watu wake wajuwe kweli na kweli iwaweke huru. Kwa nini uendeleye kushiriki katika dhehebu fulani ukisema "*kwa sababu nimekosa mahali pengine pa kwenda, wazazi wangu hawawezi nikubaliya niondoke, mchumba wangu ataniacha, wakubwa wetu watanilaani, nitapoteza faida fulani, …*".
Ama tena ni la shetani kwa kuwa yeye ni bingwa katika kufananisha ili anayoyatowa yawe na picha ya yale ya kweli ingawa si kweli kabisa. Mungu asipokufungua macho (kuzihakikisha alama zile ambazo zimetolewa), hakika wengi watapoteya katika kujifariji kwao (napenda kanisa letu, humo ndimo wazazi wangu wanashiriki, nampenda sana mchungaji fulani, linanigharamia, limejengwa vizuri sana, …). Kanisa la Kristo si la kufananisha ila la kuhakikisha kwamba ndilo wala silo, kwa mwangaza wa Agano Jipya. Ikiwa ndilo unamoshiriki (unapohakikisha alama hizo zimetolewa), ulifurahiye na kulipenda kwa kuwa lina ahadi ya kunyakuliwa na Kristo. Ikiwa silo unamoshiriki (alama hizo zote usipozihakikisha), ni huzuni (kwa kuwa si kiungo cha lile litakalonyakuliwa) ila bado kungali tumaini. Utafute lile la kweli la Kristo mahali unapoishi (nchini, mjini, mkoani ao kijijini mwako) ili uhudumu ndani. Na ikiwa utahakikisha halipo, unahitaji kufuata kwa makini haya mafundisho pamoja na kungoja mengine yanayosaidiya kila mumoja "JINSI YA KUKUSANYIKA KAMA KANISA LA KRISTO MAHALI HALIJAKUWA". Kwa lengo hili, baki ukiwasiliana na Kanisa la Kristo pa Bukavu waliochapisha mafundisho haya.

*Kumbuka:*

- Kristo alisema atalijenga kanisa lake na hakika lilionekana hapo Yerusalem.
- Bwana aliongezea kanisa kila siku wale waliokuwa wakiokolewa.
- Kristo atarudi tena kulichukuwa kanisa lake.

*Basi ndugu mpendwa,*

- ikiwa umehakikisha kwamba Kanisa ni la Kristo nalo ni moja tu,
- ikiwa umeokolewa, je umewekwa na kuishi katika kanisa hili?

Kama sivyo, leo haijakuwa nyuma zaidi kwa kufanya uamzi ulio bora ili uhakikishe kwamba Bwana atakapokuja kulichukuwa kanisa lake, nawe ukiishi maisha ya uaminifu (wala si ya unafiki), uwe na uhakika kwamba utapelekwa katika hiyo raha ya milele.

Tunawapenda sana watu walio na nia ya kuokoka ndio maana tumewezeshwa kutowa mafundisho haya kwa wote.



**Anuani za sasa**
N°76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
**BP** : 452, Cyangugu – Rwanda
**Email** : egliseduchristrdcbkv@yahoo.fr (français), klk.bukavu@yahoo.fr (swahili) et bkvdrcchurchofchrist@yahoo.fr (anglais).